


FOMU YA MKATABA WA UTENGENEZAJI WA SAMANI**A: MASHARTI MAALUM YA MKATABA**

1	MWAJIRI	VETA MAKAO MAKUU, S. L. P. 802, Dodoma - Tanzania
2	JINA NA ANWANI YA Mwajiriwa	Jina: MKUU WA CHUO -KIHONDA RVTSC Anwani: 2208 - Morogoro Simu: 023 2603734
3	ENEO LA KAZI	KIHONDA RVTSC
4	MAELEZO YA KAZI KWA UFUPI	Kutengeneza samani za vyuo viwili (2) vya wilaya ya Mbarali na Chunya
5	GHARAMA ZA KAZI	26,310,000/=
6	MUDA WA MKATABA ; ni miezi sita (6) Tangu kusainiwa kwa mkataba	Tarehe ya Kuanza Kazi 1/03/2022 Tarehe ya Kumaliza Kazi 30/09/2022
7	MASHARTI YA MALIPO:	<ul style="list-style-type: none">• 50% YA MALIPO YA KAZI HII YATALIPWA MWANZONI MWA KAZI NA 50% YA MALIPO ITALIPWA BAADA YA KAZI KUKAMILIKA.


B: MASHARTI YA JUMLA MKATABA

- 1) Mtengenezaji atapatiwa vifaa vyote vya kutengenezea samani hizi ikiwemo mbaao, vyuma na vifaa vinginevyo.
- 2) Mwajiriwa/fundi atatakiwa kutoa taarifa ya matumizi ya vifaa vyote alivyokabidhiwa kwa ajili ya kazi hii.
- 3) Mwajiriwa/fundi atalazimika kufanya marekebisho yeyote yatakayojitokeza wakati wa utekelezaji kama sehemu ya maboresho.
- 4) Mwajiri hatahusika na hasara yeyote itakayojitokeza kutokana na utaratibu mbovu wa ufanyaji kazi.
- 5) Mwajiriwa anatakiwa kutumia nguvu ya ndani na wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo katika utekerezaji wa mradi huu.
- 6) Mwajiriwa atatakiwa kufanya kazi muda wa ziada ili kuhakikisha mradi huu unakamilika ndani ya muda uliopangwa.
- 7) Mwajiriwa/fundi atasambaza samani katika kituo husika.
- 8) Uvunjwaji wa Mkataba: Mkataba utavunjwa iwapo; Mwajiriwa/fundi atashindwa kukamilisha kazi iliyotarajiwa kwa muda na ubora uliopangwa, Mwajiriwa atatakiwa kurudisha gharama zote zilizoingia.
- 9) Mkataba huu unaongozwa na sheria ya Tanzania.


MWAJIRI:

Saini: 
Jina: P. Biguma
Cheo: DG
Tarehe: 1/3/2022


MWAJIRIWA/FUNDI

Saini: 
Jina: K. Maganga
Cheo: Principal
Tarehe: 1/3/2022

SHAHIDI WA MWAJIRI

Saini: 
Jina: R. Chisumo
Cheo: CS
Tarehe: 1/3/2022

SHAHIDI WA MWAJIRIWA/FUNDI

Saini: 
Jina: O. Urio
Cheo: PO
Tarehe: 01/03/22